## 1. MTAMBO MDOGO WA KUSAFISHA MAFUTA YA ALIZETI

Usafishaji wa mafuta ya kula yatokanayo na mbegu za alizeti ni hatua inayofanyika mara baada ya hatua za awali za ukamuaji wa mbegu za alizeti na kuchuja. Ukamuaji huweza kufanyika kwa kutumia mashine za kukamua mbegu za mafuta (edible seed oil expeller) au kwa kutumia njia ya kemikali ya solvent extraction. Usafishaji wa mafuta ya alizeti ni hatua muhimu kwani inasaidia kuondoa kemikali zenye madhara kama vile free fatty acids, harufu, rangi, vyuma vinavyotokana na ukamuaji, pamoja na nta (gums). Mtambo wa kusafisha mafuta ya alizeti una zehemu kuu tatu ambazo ni:-

i. Tanki la kuhifadhia coustic soda na maji chumvi (brine solution)
ii. Tanki la kusafisha mafuta lenye vifaa kama vile heater na kipima joto (thermometer)
iii. Tanki la kuhifadhia mafuta yaliyosafishwa (Storage tank).

## 2. UMUHIMU WA KUSAFISHA MAFUTA YA ALIZETI


Kwa sasa wajasiriamali wengi wadogo na wa kati wanakumbana na changamoto kubwa ya ushindani kwani mafuta ya alizeti wanazozalisha hayakidhi ubora na hivyo kupoteza mapato kwa kulazimika kuuza bidhaa zao kwa bei ya chini. Mathalani mafuta ya alizeti yaliyosafishwa yanauzwa kwa bei ya TZS. 35,000/= kwa lita tano wakati mafuta hayo hayo yasiyosafishwa ya ujazo kama huo yanauzwa kwa TZS. 27,500/=. Hapa tunaona kuwa katika kila lita tano za mafuta yasiyosafishwa mjasiamali mdogo na wa kati anayefanya bishara hiyo anapoteza 40% ya mapato kulinganisha na yule anayeuza mafuta yaliyosafishwa. Kiwango hiki cha upotevu wa mapato ni kikubwa na kinachangia katika kuongeza hali ya umasikini na kutokukua kwa wajasiriamali wanaojihusisha na biashara hii pamoja na upotevu wa mapato kwa Serikali kwa njia ya kodi.

Pia kutokana na mafuta mengi yanayozalishwa na wajasiriamali wadogo kutokidhi viwango vya ubora, watumiaji wengi wenye kujali afya na wanaofahamu madhara ya mafuta yasiyosafishwa wamekwepa kutumia mafuta haya hivyo kuzidi kuzorotesha soko kwa wajasiriamali wadogo na wale wa kati wa mafuta ya alizeti

Kutokana na changamoto iliyopo kwenye sekta hii ndogo ya uongezaji thamani kwenye zao la alizeti ni wazi mtambo huu utakuwa na msaada mkubwa katika kuongeza mapato ya wajasiriamali pamoja na kulinda afya za walaji wa mafuta yatokanayo na mbegu za alizeti.

## 3. HATUA ZA USAFISHAJI WA MAFUTA YA ALIZETI

Usafishaji wa mafuta ya alizeti huanza mara baada ya mafuta yaliyokamuliwa kuchujwa kwa kutumia mashine ya “Filter press machine”. Mara baada ya hatua hii mafuta yaliyochujwa huingizwa kwenye mtambo na kuwekwa kwenye tanki ili uchafu mzito (slurr) uweze kutuama. Baada ya uchafu kutuama mafuta huingizwa kwenye mtambo ili kutoa uchafu usiohitajika pamoja na kuyafanya mafuta kuwa katika uhalisia yaani kuondoa hali ya asidi (neutralization) ambayo huwa kwenye mafuta.




## 4. MCHANGANUO WA BIASHARA

Ukamuaji wa mafuta ya alizeti hufanyika kwa kutumia mashine maalumu ( Screw Oil Expeller) ambayo hukamua mafuta toka katika mbegu kavu za alizeti ambapo mashine hiyo hutenganisha mafuta na mashudu. Mashine hii hukamua mbegu kiasi cha 210kgs kwa saa ambayo hutoa wastani wa lita 60 za mafuta ghafi na mashudu wastani wa 150kgs. Bei ya jumla kwa wastani ya kilo moja ya mbegu za alizeti ni Shs. 1,000.

Bei ya jumla ya Mafuta ambayo hayajasafishwa/ghafi (Onrefined Oil) Tshs. 5,500 kwa lita moja, Kwa kila saa moja mashine huingiza ingiza mapato ya Shs. 330,000, kwa Masaa nane mapato ya Mafuta ghafi/ ambayo hayaja safishwa (Unrefined Oil) itakuwa ni Shs. 2,640,000. Bei ya mashudu ni Tshs. 500/= kwa kilo, hivyo

kwa kila lisaa limoja mapato yatokanayo na mashudu ni Tshs. 75,000/= kwa masaa nane mapato ya Mashudu ni Tshs. 600,000/=. Jumla kuu ya mapato ghafi kwa siku itakuwa ni Shs. 3, 240,000.

Aidha, mafuta haya lita 60 yakisafishwa (Refined Oil) hubakia lita 54 ambayo kwa bei ya Jumla yanauzwa Tshs. 7,000/= kwa lita (sawa na 378,000/= kwa lita 54). Mapato haya ya 324,000/= ni yanayopatikana kwa saa. Hivyo kwa masaa nane mapato ghafi yatakuwa Tshs. 3,024,000/=. Uchafu unao toka/baki baada ya kusafisha Mafuta unaweza tumika kutengenezea sabuni.

**Jedwali la Mchanganuo wa Biashara**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UKAMUAJI WA MAFUTA YA ALIZETI** | | | | |
| **No** | **Gharama** | **Malighafi** | **Mchanganuo** | **Gharama** |
| **1** | Alizeti | 210Kgs | 210 x 1100 Shs x 8 Masaa x 24 Siku | 44,352,000 |
| 2 | Umeme | Uniti 19 kwa Saa | 20 uniti x400 Shs x 8 Masaa x 24 Siku | 1,536,000 |
| 3 | Mshahara - Vijana Watatu | | 3 watu x 10,000 Shs x 24 Siku | 720,000 |
| 4 | Chakula na Nauli | | 3 watu x 8000 Shs x 24 Siku | 576,000 |
| 5 | Kukodisha eneo | | | 300,000 |
| 6 | Gharama nyinginezo | | | 1,200,000 |
| | **Jumla ya Gharama** | | | **48,684,000** |
| | | | | |
| | **MAPATO** | | | |
| 7 | Alizeti | 210Kgs | 60Lts x 5,500 Shs x 8 Masaa x 24 Siku= | 63,360,000 |
| 8 | Mashudu | 150kgs | 150 x 500 Shs x 8 Masaa x 24 Siku = | 14,400,000 |
| | **Jumla ya Mapato** | | | **77,760,000** |
| | | | | |
| | **FAIDA KWA MWEZI** | | | **29,076,000** |
| | | | | |
| | | 54 Lts | 54 Lts x 7,5000 Shs x 8 Masaa | 3,240,000 |
| | | | | |
| **KUSAFISHA MAFUTA YA ALIZETI (REFINED OIL)** | | | | |
| 9 | Mafuta | 1000 Lts | 1000 Lts x 5,500 Shs X 12 Siku kwa Mwezi | 66,000,000 |
| 10 | Umeme | 22 Uniti | 22 Uniti x 8 Masaa * 12 Siku kwa Mwezi | 844,800 |
| 11 | kemikali | | | 100,000 |
| 12 | Wafanyakazi | | 2 x 250,000 Shs | 500,000 |
| 13 | Gharama nyinginezo | | | 600,000 |
| | **Jumla ya Gharama** | | | **68,044,800** |
| | | | | |
| 14 | MAPATO | | 940 Lts x 7,000 Shs x 12 Siku kwa Mwezi | 78,960,000 |
| | **FAIDA KWA MWEZI** | | | **10,915,200** |